BORN ~~GAY~~ BORN AGAIN

ZAIRE WILLIS & REGINALD ROBINSON

COMING TOGETHER MINISTRIES

CHOOSE • TRANSFORM • BELONG

# KUACHANA NA MAISHA YA USHOGA NA KUZALIWA UPYA



## Upendo wa Mungu

### Ujinsia na Utambulisho

Kipeperushi cha Huduma za Coming Out Ministries

*"Wewe ni wa maana una nafasi na unapendwa"*

*Anatuita tutoke gizani na kuingia katika nuru yake ya ajabu*
*- Petro wa Kwanza 2:9*

MaarifaMtandaoni.com, SamaritanLaymenMinisitries.Org

Asante kwa Baba wa Mbinguni na wahusika wengine

- Grace Momadi-Masaka-New Jersey, Marekani
- Martha Swamila-Dar Es Salaam, Tanzania
- Daniel Nyangaresi Masaka-Kisii, Kenya
- John and Judi Mugane-Boston, Marekani
- Denis Momadi Masaka-Oklahoma, Tanzania
- Sharon Ondieki-Nairobi, Kenya
- Jabez Masaka-Carolina, Marekani
- Musa Budodi-Shinyanga, Tanzania
- Sandra Barron-Carolina, Marekani

## SEHEMU YA KWANZA

Imefika wakati wa kuwa na huduma ya kusaidia watu wenye changamoto za ushoga ambazo wengi wamejitumbukiza kwaajili ya kutafuta fedha, msukumo wa rika, ukoloni mamboleo au kuigiza maisha ya magharibi-fake life. Tunajua zamani mwanaume alidharaulika sana kama angetaka kuwa mwanamke, wavulana na hata wanaume wengi ukiwaambia kama hebu njoo nikusuke, au vaa hii nguo, walisema, mimi siyo mwanamke, na hata kuwa mwanamke kwa wanaume lilikuwa ni tusi kubwa sana. Watu wengi walipongomana, walitukanana 'mwanamke wee', na kwa wengi, mwanamke aliyeheshimiwa, alikuwa ni mama tu, wanawake wengi walidharaulika sana. Hivyo hali iliyoletwa hivi karibuni, imeanza kubadilisha mambo mpaka kufikia hatua ya wanaume fulani kutaka kuwa wanawake ili kujikimu kimaisha au kukabiliana na msukumo wa rika. Watu wamefanyiwa hata upasuaji ili wabadilishe jinsia yao. Kumekuwa na kuchanganyikiwa kwingi katika jumuiya yetu. Nchi kama Thailand na Ufilipino walisema ziliongoza kwa upasuaji wa kubadilisha jinsia, ila mambo haya yalikuwa bado kufika kwetu. Sasa muafaka siyo kuzika vichwa vyetu kwenye mchanga, ila kuwasaidia vijana wetu, au watu wazima, kujua wao ni nani, wameumwa na nani, na wanaenda wapi, au yule aliyewaumba ana kusudi na malengo gani nao. Kila mtengenezaji wa kitu ana kanuni ya utumiaji wake, yaani user manual, Muumbaji wa jinsia alikuwa na malengo gani katika kuumba jinsia mbili? Je, kwanini watu wanasema siku hizi kuna jinsia 72! Je, mtoto akizaliwa huwa tunaona jinsia gapi, maana jambo hili siyo siri?

Tumefahamiana na wahusuka wa Coming Out Ministries, kwa zaidi ya miaka 20 walipotoa kaseti zao za kwanza na kisha kuandika kitabu chao cha kwanza, 'This Kind Never Changes- Watu Hawa wa Ushoga huwa Hawabadilikagi' sasa wanaandika vijuzuu na kutoa video nyingi, wametupa vijuzuu vyao kila mwaka ili tutafsiri tulipokutana nao, na ni kama miaka kumi sasa, ndiyo tumeona tutafsiri angalau vitano wakatupa vijuzuu vyao angalay vitano katu ya 10 na kitabu ili tutafsiri. Soma kwa Kiingereza haya mambo kwa undani zaidi kwani wana mengi ya kusema na video za Youtube ili uwasaidie wengi kutoka kwenye mtindo wa maisha wa giza na kuingia nuruni.

## Utambulisho Wangu ni Upi

Je, Mungu ananipenda ikiwa ninavutiwa na mtu wa jinsia yangu\moja? Vipi kuhusu watu wanaojitambulisha kuwa sehemu ya jumuiya ya LGBT+? Ikiwa Mungu ni upendo, kwa nini ni kosa kumpenda ninayempenda? Ninawezaje kumpenda mwanangu wa kiume au wa kike ambaye ni shoga? Je, nihudhurie harusi yake? Nimrejeleeje mtu anayejitambulisha kwa jinsia tofauti na ile aliyopewa wakati wa kuzaliwa? Katika utamaduni unaosisitiza haki yetu ya kuamua ujinsia wetu wenyewe, tunawezaje kuwasilisha upendo wa Mungu kwa namna isiyokera na ambayo bado ni ya kweli?

Huduma za Coming Out ni huduma inayotegemea Biblia na inayolenga kuwasaidia watu kupata majibu kuhusu ujinsia wao na namna wanavyoeleza utambulisho wao. Unaposoma kipeperushi hiki, tunakusudia kusaidia kufafanua upendo wa kweli ni nini na jinsi unavyotenda kwa mtazamo wa Biblia.

## Mungu ni Upendo

> *"Mungu ni upendo." (Yohana wa Kwanza 4:16).*

Kwa kuwa Mungu ni upendo, angekuwa anajipinga ikiwa asingewapenda watu wote. Hii inawajumuisha watu wa jumuiya ya LGBTQ+.

Hapo awali, sisi katika Huduma za Coming Out hatukujua kwamba upendo wa Kristo ulikuwa ukituita. Hatukuwa na hamu ya kumjua Mungu tuliyedhani alikuwa ametukataa, Mungu aliyedai tuyakane mavutio tuliyoamini ndiyo yaliyotutambulisha. Tulisema, "Usiniombee; sijavunjika."

Yesu alitumia njia gani kuwashawishi wengine na kuwavuta katika upendo wake?

## SEHEMU YA PILI

Njia ya Kristo ya Kuwafikia Watu

> *"Mbinu ya Kristo pekee ndiyo itakayotoa mafanikio ya kweli katika kuwafikia watu. Mwokozi alichangamana na watu kama mtu aliyewatakia mema. Aliwaonyesha huruma, akawahudumia mahitaji yao, na akapata imani yao. Kisha akawaambia, 'Nifuateni.'" (Huduma ya Uponyaji, uk. 143).*

Kukutana na Watu Walipo

Ni muhimu kuwakuta watu mahali walipo, bila kuwadharau wala kuwaonyesha karaha. Yesu anatukuta tulipo katikati ya mkanganyiko, kukataliwa na chuki. Kisha hushughulikia majeraha ya kukataliwa yaliyopita au ombwe linalotokana na kutowahi kumjua Mwokozi mwenye upendo na huruma, ambaye hataki jambo lolote zaidi ya mema yetu.

Kujenga Urafiki

Kujenga urafiki ni hatua ya kwanza. Kutenga muda wa kumjua mtu binafsi kunaweza kujenga imani na kuaminiana, na kuonyesha upendo unaofanana na wa Kristo. Ukiwa na mtazamo mpole usio wa kujiona, usitoe hukumu za haraka; mtendee kwa heshima na moyo wa unyenyekevu kila mtu unayemkaribia.

Omba uongozi wa Roho Mtakatifu. Usichukue hatua wala kusema neno bila kuliweka kila tukio mbele za Mungu kwa maombi. Ujue kwamba jitihada zako zitaambatana na nguvu na huruma.

## SEHEMU YA TATU

Kutengeneza Biskuti

Binti wa rafiki yangu ambaye ni shoga aliomba kurudi nyumbani mwishoni mwa juma. Mama yake alifurahi kufikiria kwamba binti yake angerudi nyumbani kwa ziara. Hata hivyo, alishtuka na kuvunjika moyo binti yake alipouliza kama angeweza kuja pamoja na mpenzi wake wa kike.

> *"Sitaki mwanamke huyo nyumbani kwangu," alisema mama yake, "wala sitaki kuwaona wakigusana mbele yangu au kufikiria mambo anayofanya na binti yangu."*

Baada ya kuomba, alisadiki kwamba ubaguzi wake haukuwa sahihi na kwamba mpenzi wa binti yake pia alikuwa mtoto wa Mungu. Kwa wasiwasi, alimwambia binti yake kwamba angeweza kuja naye, lakini walipaswa kulala katika vyumba tofauti na kutoonyesha mapenzi mbele ya wengine. Binti yake alikubali masharti hayo na akamleta mpenzi wake kwa ajili ya mwisho wa juma. Mama alijitahidi sana kutoonyesha masikitiko yake na akamruhusu Roho Mtakatifu afanye kazi moyoni mwake.

Jumapili asubuhi walipoamka, binti alimwambia mama yake, "Tunaweza kupata biskuti za Kimarekani na mchuzi?" Jibu la kwanza la mama lilikuwa kuandaa kifungua kinywa walichoomba, lakini akatambua kwamba angehitaji msaada. Bila kusita, aliwaomba binti yake na mpenzi wake wamsaidie. Binti yake alisema, "Unataka nifanye nini? Mpenzi wangu hajui kupika." Mama akamtazama yule msichana na kusema, "Basi nitakuonyesha jinsi ya kutengeneza biskuti au maandazi."

Baada ya chakula kuandaliwa, sahani kuoshwa na kuwekwa mahali pake, wasichana wale wawili walitoka nje kutembelea shamba. Mama alikuwa ndani ya nyumba, na wasichana walipokuwa ghalani, mpenzi wa binti alianza kulia kwa kwikwi ghafla. Binti alipoona amevunjika moyo, akamuuliza, "Kuna nini?"

> *"Siwezi kuamini jinsi mama yako alivyo mwema kwangu," alisema yule msichana. "Kwa nini anifundishe kupika wakati mama yangu mwenyewe hakunifundisha? Ninajua mama yako hakubaliani na uhusiano wetu, lakini siwezi kuacha kushangazwa na jinsi alivyonipenda. Huu ni upendo mwingi kuliko niliowahi kupata kutoka kwa mama yangu mwenyewe!"*

## Upendo Unaonekana Katika Maisha

Mama hakujua angewezaje kuleta mabadiliko katika maisha ya binti yake au ya mpenzi wa binti yake. Lakini alipojisalimisha kwa Roho Mtakatifu, alimwongoza. Wema na upendo alioonyesha asubuhi hiyo vilikuwa na athari kubwa kwa wanawake hao wawili vijana.

Hivyo ndivyo Yesu alivyohudumu. Njia yake yenye huruma inapinga dhana za awali za mwenye mashaka kuhusu dini na ujinsia. Ikiwa tunataka kuleta mabadiliko katika maisha ya wengine, wanahitaji kuona nguvu ya upendo wake ikifanya kazi katika maisha yetu wenyewe.

## Kuhusu Huduma za Coming Out

Journey Interrupted ni filamu ya hali halisi yenye ujumbe wa ukombozi, inayoonyesha nguvu na huruma ya Mungu kupitia safari za timu ya Huduma za Coming Out. Shuhuda mbalimbali zinazomo zinajadili ujinsia kwa namna mpya na inayotegemea Biblia.

*journeyinterrupted.com*

Huduma za Coming Out zinatambua huruma ya Kristo katika kuwahudumia wanaume na wanawake wanaokabiliana na mkanganyiko kuhusu ujinsia na utambulisho. Lengo letu ni kuwa daraja la kuwafikia watu wa jumuiya ya LGBT+, na pia kulihamasisha, kulielimisha na kuliandaa kanisa kukabiliana na changamoto za utamaduni huu.

Huduma hizi hushughulikia ujinsia na usafi wa maisha kwa watu wa umri wote, pamoja na uraibu wa ponografia na masuala mengine ya kingono. Huduma za Coming Out hutoa huduma ndani ya nchi na kimataifa. Ili kupanga wasilisho katika kanisa au tukio lako, wasiliana nasi kupitia anwani ifuatayo.

*comingoutministries.org*